بسم الله الرحمن الرحيم

KUOA WAKE WENGI (UKE WENZA)

I- MAANA YA UKE WENZA:

Ni Mume kuowa zaidi ya mke mmoja hadi wanne na kuwa nao pamoja katika ndoa.

II- HISTORIA FUPI YA KUOA WAKE WENGI ?

Haukuwa Uislamu ndiyo dini ya kwanza kuruhusu kuoa wake wengi na wala Uislamu haukuzua utaratibu huu.

Bali Uislamu umekuwa ndiyo dini ya kwanza kuratibisha na kuyawekea utaratibu mzuri masuala ya ndoa. Isitoshe Uislamu ukaliwekea suala la kuoa wake wengi masharti madhubuti na magumu, ambayo Mume analazimika kuyazingatia kabla ya kuongeza mke/wake.

Suala la kuoa wake wengi halikuwa tu ni ada na desturi za waarabu zama za jahiliya, bali pia ilikuwa ni desturi ya mataifa mbalimbali kwa namna moja au nyengine, kama historia inavyokiri ukweli huu.

Historia inaonyesha kuwa hata hapa kwetu Tanzania, watemi (machifu) wa makabila mbali mbali bali watu wa kawaida wenye mali walikuwa na wake wengi, huu ni ukweli usiopingika.

Utaratibu huu wa kuoa wake wengi ulikuwemo pia katika vitabu vilivyoitangulia Qur-ani Tukufu.

Mna ndani ya Taurati maandiko na matukio yanayouthibitisha ukweli huu na wala hamna ndani ya Injili aya/maandiko yanayoharimisha kuoa wake wengi.

Kulingana na Uyahudi na ukitazama hasa katika Agano la Kale utakuta kuwa Manabii watukufu wengi walikuwa na zaidi ya mke mmoja kwa mfano Abrahamu alikuwa na watatu, Daudi mia moja, Suleiman mia saba, Yaaqub wanne na wengineo.

Nae bwana Mtume Muhammad Alaihi Salam aliwakusanya wake tisa wakati mmoja.

Bali kuoa wake wengi kulizuiliwa na kanisa katika karne ya kati {karne ya 10-15 AD} na wakati mwingine waliruhusiwa na kanisa baadhi ya wafalme wakubwa kuoa wake wengi. Rejea vitabu vya historia ya kanisa.

III- UISLAMU UMERUHUSU KUOA WAKE WENGI KWA SHARTI:

1. Isizidi idadi yao wake wanne
2. Kufanya uadilifu baina yao.

Makusudio ya uadilifu ni kufanya usawa kati ya wake zake mtu katika huduma, mavazi, zamu, chakula na mengineyo katika huduma anazoweza.

Ama uadilifu katika mapenzi basi sharia haimkalifishi kwa sababu hatoweza kama anavyobainisha hayo Allah

{وَلَن تَسْتَطِيعُواْ أَن تَعْدِلُواْ بَيْنَ النِّسَاء وَلَوْ حَرَصْتُمْ فَلاَ تَمِيلُواْ كُلَّ الْمَيْلِ فَتَذَرُوهَا كَالْمُعَلَّقَةِ وَإِن تُصْلِحُواْ وَتَتَّقُواْ فَإِنَّ اللّهَ كَانَ غَفُوراً رَّحِيماً }النساء129

"Wala hamtaweza kufanya uadilifu baina ya wake, hata mkikakamia. Kwa hivyo msimili moja kwa moja mkamwacha (mmojapo) kama aliye tundikwa. Na mkisikizana na mkamchamngu basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira na Mwenye kurehemu" (4:129)

3. Uwezo wa kuwahudumia wake wengi. Kwa kuwapa mahitaji yao ya lazima kama makazi, chakula ,mavazi, matibabu nakadhalika. Na kama hana uwezo basi haifai kwake kuongeza mke. Kama anavyosema Allah Mtukufu:

{وَلْيَسْتَعْفِفِ الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحاً حَتَّى يُغْنِيَهُمْ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ }النور33

"Na wajizuilie na machafu wale wasio pata cha kuolea, mpaka Mwenyezi Mungu awatajirishe kwa fadhila yake" (24:33)

IV- HUKUMU YA UKE WENZA:

Inafaa kuoa mke Zaidi ya mmoja kwa dalili zilizothibiti katikaTunasoma ndani ya Qur-ani Tukufu na hadithi za Bwna Mtume Swalallahu alaihi wasalam.

Allah anasema katika Qur-ani:

{ فَانكِحُواْ مَا طَابَ لَكُم مِّنَ النِّسَاء مَثْنَى وَثُلاَثَ وَرُبَاعَ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلاَّ تَعْدِلُواْ فَوَاحِدَةً أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ذَلِكَ أَدْنَى أَلاَّ تَعُولُواْ }النساء3

"…. Basi oeni mnaowapenda katika wanawake (maadam mtafanya uadilifu) wawili au watatu au wanne (tu). na mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu, au (wawekeni masuria) wale ambao mikono yenu ya kuume imewamiliki. kufanya hivyo ndiko kutapelekea kutofanya ujeuri." [4:3]

Mtume – Rehema na Amani zimshukie – alimwambia Ghaylan At-thaqafiy, ambaye alisilimu akiwa na wake kumi

"Kaa na wanne (tu) miongoni mwao na waache (wataliki) waliosalia" At-tirmidhiy, An-nisaai na Ibn Maajah. Ni vema ikafahamika kwamba huyu Ghaylan alikuwa ndiye mtemi (mfalme) wa Twaif.

Suala hili la kuoa wake wengi ni suala lililofanywa na mwenyewe Bwana Mtume, maswahaba na waliokuja baada yao na ni suala ambalo umma mzima wa kiislamu umekongamana juu yake.

Uke wenza katika uislamu unajumuisha hukumu tano za kisheria, nazo ni:

1- halali: Kwa yule mwenye uwezo na haja ya kuoa Zaidi ya mke mmoja hadi wa nne na atakuwa muadilifu.

2- Wajibu: Ikiwa kuna jambo la lazima kuongeza mke mfano katoka hali zifuatazo:

a) Kutaka kizazi ikiwa mkewe ni tasa.

b) Mke Mgonjwa ambae anapoingiliwa anapata madhara. Mume ataongeza mke (ikiwa hawezi kusubiri) ili kujihifadhi zina.

3- Sunna: Kwa yule mwenye uwezo wa mali na mwili pamoja na kuweza kuwafanyia uadilifu wake zake na akataka kwa sababu ya kisheria kama kuongeza wingi wa watu, au kupunguza wajane, au kuogopa kuingia makosani kwa kutotosheka na mke mmoja.

4- **Makruhu:** Kwa yule mwenye uwezo wa mali na mwili lakini akahisi kuwa hatoweza kufanya uadilifu baina ya wake wengi.

5- Haramu: Ni kwa yule asiekuwa na uwezo wa mali juu ya kuowa au kwa yule aliekuwa hana nguvu za kiume na uwezo wa kumtosheleza mkewe au wakeze, au yule mwenye uhakika kuwa hatoweza kufanya uadilifu kwa wakeze, au kwamba atamdhulumu mkewe na wala hana haja ya kuowa mke mwengine.

V- HEKIMA /SABABU YA KUOWA WAKE WENGI

Ukweli ni kuwa si kila kitu kimeelezwa hekima yake lakini Wanachuoni wanajitahidi kuangalia hekima ya mambo kadhaa ambayo yamo katika Qur-aan Tukufu au Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam). Hivyo, Imani ya Muislamu ni kuwa hata asipopata hekima ya amri au katazo fulani basi yeye huwa ni mwenye kusema: *“Tumesikia na tumetii”* (2: 285).

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

{وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْراً أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالاً مُّبِيناً }الأحزاب36

" *Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi"* **(33:36).**

Sheria hii inayomruhusu mwanaume kuoa zaidi ya mke mmoja ina Faida na manufaa kwa wote wawili; mwanamume na mwanamke na jamii kwa ujumla.

a) Kwa upande wa mwanamme :

i. Mke kutomtosheleza mume haja yake ya maumbile. Hili husababishwa na uwezo mkubwa wa mume katika tendo la ndoa na udhaifu wa mke. Mume hataki kumuacha mkewe, sasa ataitosheleza wapi kiu yake ? Hapo ndipo uislamu ukamruhusu kuoa mke mwingine na yule wa mwanzo kubakia pale pale.

ii. Mwanamke kuwa tasa; hazai na mume anatamani kupata watoto, ambalo hili la kupata watoto ni mojawapo ya malengo na madhumuni ya ndoa. Lakini mume anampenda mkewe na kwa sababu moja au nyingine hataki kumuacha.

iii. Hali ya Kimaumbile ya mwanamke: Upo wakati mrefu ambapo mwanamke hawezi hutekeleza majukumu yake ya kindoa kwa mabadiliko ya kisaikolojia na kifiziolojia na kimwili kama wakati akibeba mimba, hedhi na nifasi, na huku mume ana matamanio ya kufanya tendo la ndoa, sasa akafanye wapi? Uke wenza inawezakuwa moja ya kutatua tatizo hilo.

iv. Hali ya safari kwa mume: Inawezekana mume kupata safari ya mbali kikazi au kimasomo na akawa mbali na nchi yake na ikawa vigumu kumsafirisha mkewe, na akashindwa kujizuia na

matamanio yake, kwahio kitendo cha kuoa mke mwengine huko aliko itakua ndio maslahi kwake kuepukana na maasi.

v. Kuepusha kutoa talaka kwa ajili ya kulinda watoto na familia. Inawezekana pakatokea sitofahamu kati ya wanandoa wawili, na mume akaamua kutotoa talaka kwa ajili ya kuwahifadhi watoto wake kupotea na kusambaratishwa na mbadala wake akaowa mke mwengine na mkewe wa mwanzo kubaki naye.

Haya ni baadhi tu ya maslahi ya sheria hii ya kuoa zaidi ya mke mmoja kwa upande wa mume.

b) Kwa upande wa mwanamke:

Hebu tuangalie mwanamke naye, ananufaika vipi na sheria hii :

i. Kulinda heshima ya Mwanamke: Inawezekana kabisa mke akapatwa na maradhi yakamsababishia kushindwa kabisa kuitekeleza haki ya unyumba kwa mumewe. Maskini mke huyu mgonjwa, aende wapi na il-hali sasa katika kipindi kigumu cha ugonjwa ndio anahitajia zaidi huruma, mapenzi na liwazo la mumewe.

Mumewe amtaliki ? La, hapana, sheria inambana mume kuwa katika mkataba wa ndoa alichukua ahadi kuishi naye katika raha/shida, uzima/ugonjwa, basi amuuguze mkewe na ili kukidhi haja zake za kimaumbile basi na aoe mke mwingine, Je hapo mwanamke hajanufaika?

ii. Kumuepusha mwanamke na madhara: Inafahamika kuwa binadamu anatofautiana katika sura, akili, tabia na kadhalika. Ni kama hivyo pia tunatofautiana katika uwezo/nguvu ya kujamiiana. Inaweza uwezo wa mume ukawa ni mkubwa sana kuliko mkewe, mume ni tembo na mke ni kondoo, vipi kondoo atahimili vishindo vya tembo ? Sasa, ili mke huyu asiichukie ndoa na hatimaye kukimbia, uislamu ukamruhusu mume kuongeza mke mwingine. Siku za zamu ya mke mwingine, huyu asiyehimili vishindo atapata kupumzika. Hebu tuwe wakweli, mwanamke huyu kanufaika au la?

iii. Kumuepusha Mwanamke na Maradhi ya Zinaa: Mume anapokua na mke mmoja na akiwa hamtoshelezi na akashindwa kujizuia na matamanio yake huenda ikampelekea kutafuta wanawake wan je kuzini nao na kupelekea kupata maradhi ya zinaa kama ukimwi n.k, lakini atakapokuwa na mke Zaidi ya mmoja itakuwa kinga ya kutosheleza matamanio yake na kujiepusha na maradhi hayo.

c- Maslahi ya Uke wenza kwa jamii:

i- Kupunguza wingi wa wajane: Hakuna jamii isiyokuwa na wajane na mayatima; ambao hawa wanataka wapate uangalizi na malezi. Inawezekana sababu yake ikiwa ni kutokana na vita, au majanga ambayo wahanga zaidi huwa wanaume na kusababisha wanawake kubakia wengi Zaidi. Nani basi atawalea wajane hawa waliofiwa na waume zao na hawa walioachwa na baba zao ? Hapo ndipo Uislamu ukampa ruhusa mwanaume ambaye tayari ana mke, kuongeza mke mwingine. Pengine huyu atakayemuoa ni huyo mjane, mwenye mayatima.

ii- Takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya wanawake duniani ni kubwa kuliko idadi ya wanaume. Haya ni matokeo ya utafiti uliofanywa na taasisi mbali mbali ulimwenguni kote. Sasa itakuwa tunakubaliana na takwimu hizi na leo vita vimetapakaa duniani kote na wahanga (wa vita hivi, wengi wao ni wanaume kwa kuwa wao ndio askari wanaopigana vita.

Hebu tuchukulie/tukadirie kuwa uwiano wa wanaume na wanawake duniani 1:5 yaani mwanaume mmoja kwa wanawake watano. Sasa ikiwa kila mmoja akioa mke mmoja hawa waliobaki waende wapi, wakaolewe na nani ? Kwa kuzingatia hili ndio uislamu ukamruhusu mwanaume kuoa mke zaidi ya mke mmoja kwa sharti ya kuwa awe muadilifu baina yao.

iii- Kufuata sunna ya Mtume Rehema na Amani zimshukie juu yake ambae aliowa wake wengi na masahaba nao kuiga mwendo wake , jambo ambalo limepelekea jinsi mwanamke wa kiislamu alivyohifadhika, wajane wa vita pia nao hawakutupwa mkono, na Mtume – Rehema na Amani zimshukie – ndiye aliyeanza kuonyesha mfano.

Je, tuna mfano mkubwa kuliko wa Mtume wakati Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuamrisha tumfuate ?

Tunafuata mkumbo wa maadui wa kiislamu unaodai haki za wanawake na kushikilia kuoa mke mmoja, pamoja na kuweka vimada, kumvunjia mwanamke heshima yake kwa kumvua nguo na kumtumia kwenye matangazo ya biashara, madansa, miss world na kadhalika.

Leo mwanamke akiolewa ananyang'anywa hata jina la mzazi wake na kujulikana kwa jina la mumewe, Mrs fulani, sasa ni nani anayemtakia mema mwanamke, Mwenyezi Mungu aliyemuumba au wakazi wa dunia hii wakiongozwa na mwanaume ambaye yuko tayari kufanya lolote kutekeleza matashi ya nafsi yake ???

iv. Kuongeza wingi wa idadi ya wafuasi wa Umati wa Mtume Muhammad: Kama alivyotuhimiza Bwana Mtume kwa kusema: Oweni wanawake wenye mapenzi wenye kuzaa sana kwani mimi nitajifakharisha kwenu kwa wingi wenu" Imepokewa na Nassai.

VI- MADHARA YA KUKOSEKANA UKE WENZA

Kuna madhara makubwa yanapatikana katika mataifa na jamii bali na watu yanayotokana kwa sababu ya kuzuiwa uke wenza kama vile:

i. Kuenea machafu ya zinaa, usagaji na Liwati.

ii. Kukithiri watoto wa Zinaa na kupelekea Kupoteza nasabu zao na kusababisha kutelekezwa na kukosa haki zao za kimsingi.

iii. Kukosekana maadili mazuri katika jamii.

iv. Kuenea madanguro na machangudoa wanaojiuza katika jamii.

VII- KWA NINI MWANAMKE ASIOLEWE NA WANAUME WENGI?

1. Ni hakika kuwa maumbile ya mwanamke kisaikolojia na fiziolojia ni tofauti na mwanaume. Kisaikolojia ni kuwa mwanamke anatosheka na mume mmoja. Kifiziolojia mwanamke hawezi kujimudu kuwa na wanaume zaidi ya mmoja kwa sababu ya mabadiliko ndani ya mwili wake.

2. Katika tamaduni zote, za zamani na sasa, uongozi wa nyumba (familia) ni wa mwanaume. Unaweza kufikiria katika familia ambayo ina kiongozi zaidi ya mmoja, nyumba hiyo itaendeshwa vipi? Ndio wahenga wakawa na msemo: "Fahali wawili hawakai kwenye zizi moja".

3. Mwanamke huyu ataweza vipi kuwaridhisha wanaume hao wote katika chakula na mapenzi. Tuseme kuwa utawagawia siku, mmoja wao anakuja na mke huyo yuko katika hedhi naye ana shauku ya juu sana, atafanyaje? Je, mke atachukua amri kutoka kwa nani?

4. Mke anayeolewa na mume zaidi ya mmoja, anaposhika mimba itakuwaje? Mtoto huyo atakuwa wa nani?

MAREJELEO:

1. القرآن الكريم برواية حفص.
2. الجامع الصّحيح سنن التّرمذيّ :لمحمّد بن عيسى أبي عيسى التّرمذي السّلميّ (209 - 279 هـ) / تحقيق أحمد محمّد شاكر وآخرون/ دار إحياء التّراث العربيّ/ بيروت.
3. سنن ابن ماجه :لمحمّد بن يزيد أبي عبد الله القزويني(207- 275هـ) / تح:محمّد فؤاد عبد الباقي / دارا لفكر.
4. سنن النّسائيّ الكبرى: لأحمد بن شعيب أبي عبد الرّحمن النّسائي (215-303)/ تح:د. عبد الغفار سليمان البنداري وغيره/ دار الكتب العلميّة / بيروت/ ط.1/ 1411هـ - 1991م .
5. الأمّ: لمحمّد بن إدريس الشّافعيّ أبي عبد الله(150-204هـ) / دار المعرفة/ بيروت/ط.2/ 1393هـ.
6. لطائف النساء/ رضا ديب/ دار الكتب العلمية/ بيروت/ط.1/ 1421ه-2000م.
7. المرأة بين طغيان النظام الغربي ولطائف التشريع الرباني/ د. محمد سعيد رمضان البوطي/ دار الفكر/ دمشق/ ط1427/7هـ - 2006م.

- www.uislamu.org/.../363-kwa-nini-uislamu-umeruhusu-kuoa-wake-wengi
- http://www.alhidaaya.com/sw/node/713
- https://mawdoo3.com/
- https://islamqa.info/ar/answers/14022
- https://www.alukah.net/sharia/0/124445/#_ftnref10

Imetayarishwa na :

Shk. Ali Muombwa Hassan
Ofisi ya Mufti- Zanzibar.
05/09/2020